CHAMA CHA MAPINDUZI

KANUNI ZA UTEUZI

WA WAGOMBEA WA

CCM KATIKA VYOMBO

VYA DOLA

(TOLEO LA Februari, 2005)

Zimetolewa na:

Halmashauri Kuu ya Taifa

Dodoma

“Madhumuni na lengo Kuu la CCM ni hili:
Kushinda katika Uchaguzi wa Serikali Kuu na Serikali za mitaa Tanzania Bara na Zanzibar ili kuunda na kushika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar”.

(KATIBA YA CCM 1997)

UTANGULIZI

(I) CCM ni Chama cha Siasa nchini chenye historia ndefu ya mapambano na uwezo mkubwa wa kuongoza Taifa kutokana na kukubalika kwake na wananchi. Hivyo kina wanachama wengi, kina Katiba, Itikadi ya Siasa, Sera za uwazi na ukweli, miongozo na Ilani mbili za Uchaguzi unaofanywa na wananchi. Ilani hizo ni:-

(1) Ilani ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hususan Madiwani;

(2) Ilani ya Uchaguzi wa Serikali Kuu

(II) Chaguzi hizo zote hufanyika kwa mujibu wa Katiba ya Nchi chini ya Sheria zetu za Uchaguzi. Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Serikali au Uchaguzi Mdogo wowote unaofanywa kwa lengo la kuziba pengo lolote la uongozi, nafasi za uongozi katika vyombo vya Dola ambazo raia wa Tanzania huchaguliwa kushika ni hizi zifuatazo:-

(1) Mwenyekiti wa Kitongoji

(2) Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

(3) Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

(4) Diwani wa Kata (Bara) au Wadi (Zanzibar);

(5) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi (Tanzania Zanzibar);

(6) Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(7) Rais wa Zanzibar;

(8) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (na Makamu wa Rais);

(9) Madiwani, Wawakilishi na Wabunge wa Viti Maalum Wanawake.

(III) Kwa kuzingatia maadili ya ushindani wa Kisiasa unaoambatana na mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa, Chama Cha Mapinduzi kitateua jina moja tu la mwanachama wake atakayesimama kugombea kila nafasi wazi iliyopo kati ya hizo. Isipokuwa kwamba kwa nafasi za ujumbe wa Halmalshauri ya Kijiji, Chama kitateua idadi ya wagombea wanaolingana na idadi ya nafasi wazi zilizopo za ujumbe huo. Kuhusu Madiwani, Wawakilishi na Wabunge,Viti Maalum na Wabnge wa uwiano, Chama kitateua/kitapendekeza idadi ya wagombea wa kila nafasi idadi inayotakiwa kwa mujibu wa sheria.

(IV) CCM ni tofauti sana na vyama vingine vya siasa nchini ambavyo vina usajili kamili chini ya sheria ya Vyama. Sifa pekee za CCM zinajidhihirisha wazi wazi katika masuala mazito ya kitaifa yafuatayo:-

(1) Azma ya kuhakikisha kwamba Muungano wa Tanzania “na Mapinduzi ya Zanzibar vinaheshimiwa, vinalindwa na vinaendelezwa wakati wote.”,

(2) Azma ya kuhakikisha kwamba ardhi inaendelea kuwa rasilimali kuu ya Taifa na inayoendelezwa kwa maslahi ya wananchi wote.

(3) Azma ya kutaka kuona kwamba Tanzania ni Taifa lenye Umoja, Amani, Utulivu na Mshikamano madhubuti wa kitaifa wakati wote;

(4) Azma ya kuhakikisha kwamba Utawala wa Sheria na Utawala Bora vinalindwa na kuendelezwa wakati wote;

(5) Azma ya kuhakikisha kwamba Watanzania tunajenga maadili na demokrasia ya vyama vingi katika mazingira ya amani, *yanayokataa* siasa za uchochezi, uzushi, kashfa, uzandiki, uongo, ubaguzi wa rangi, ukabila, umajimbo na udini, mambo ambayo ni kinyume cha Haki za Binadamu.

Wananchi kuichagua CCM maana yake ni kujihakikishia wao wenyewe kwamba wataendelea kula hayo matunda ya uhuru kwa ukamilifu.

(V) Kanuni hizi ni mwongozo kwa vikao vya CCM vinavyochuja na kufanya uteuzi wa mwisho wa Makada wa CCM ambao hujitokeza kuomba kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika vyombo vya Dola. Lengo la Kanuni ni kurahisisha utaratibu wa Chama katika kuamua nani agombee na nani asigombee katika mazingira ya demokrasia, uwazi na ukweli. Aidha Kanuni hizi ni dira kwa wanachama wa CCM ambao wana uwezo, nia, matumaini na sifa bora za uongozi ili wakati wa uchaguzi waweze kuomba kugombea nafasi hizo za uongozi bila ya kubabaika.

FUNGU LA KWANZA

KANUNI ZA JUMLA

MASHARTI YA UONGOZI KATIKA SERIKALI

1. Kila Kada wa CCM anayegombea na hatimaye kuchaguliwa kushika nafasi yoyote ya uongozi katika Serikali anapaswa kukiri kwa dhati kwamba maendeleo halisi ya wananchi yanayosimamiwa na Serikali ya CCM katika kipindi kinachohusika, yanapatikana kwa njia ya utekelezaji uliokamilika wa ILANI za CCM za uchaguzi. Kwa hiyo wajibu wake wa kwanza ni kusimamia utekelezaji wa ILANI zetu katika eneo lake la uongozi kwa uwezo wake wote.

2. Kiongozi wa kuchaguliwa mwenye madaraka ya utawala **-** Kwa mfano Mwenyekiti wa Kitongoji, Mtaa, Kijiji au Rais wa Nchi - ana wajibu wa kuhakikisha kwamba kazi zote za Serikali katika ngazi yake zinafanywa kwa ukamilifu kwa kufuata Taratibu, Sheria na Kanuni za Utumishi Serikalini. Kanuni hii ina umuhimu wa kwanza na pia wa pekee katika utekelezaji wa kazi za Serikali chini ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Bila ya kufuata Taratibu, Sheria na Kanuni, Utendaji kazi Serikalini utatawaliwa sana na malumbano ya kisiasa, vurugu, majungu, uzembe, wizi, rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, mambo ambayo ni kikwazo kikubwa katika harakati za ujenzi wa Taifa.

3.(1) Kiongozi wa Serikali ya CCM ambaye pia ni Mwakilishi wa wananchi **-** kwa mfano: Diwani, Mbunge, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi - ana wajibu mkubwa sana katika kuhakikisha kwamba:-

(i) Anatembelea Jimbo lake na kukagua mara kwa mara utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo imetengewa fedha ili aone mwenyewe na kufanya tathmini ya viwango vya utekelezaji ambavyo vimefikiwa. Lengo hapa ni kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo ili iweze kukamilishwa katika muda uliopangwa pamoja na kuzuia au kukomesha utekelezaji hewa wa miradi ya maendeleo kwa jumla. Tathmini hiyo ndiyo msingi wake na sababu ya kuihoji Serikali juu ya utekelezaji wa shughuli za Serikali zinazofanyika katika Jimbo lake.

(ii) Kuwatembelea mara kwa mara wananchi wa Jimbo lake ili kujielimisha juu ya ubora wa maendeleo yao kiuchumi na kijamii, kujua kero zao ili aweze kushiriki kwa ukamilifu katika kuzitatua; kusanifu mambo hayo na kuyajengea hoja zenye mwelekeo wa kuongeza kasi ya maendeleo ya wananchi waliomchangua. Kazi hii sharti ifanyike kwa kipindi chote cha miaka mitano ya Uwaklishi wake.

(iii) Kuwa karibu na kushirikiana vizuri na ngazi zote za vyombo vya Serikali, NGO's na Taasisi nyingine, vinavyosukuma siku hadi siku maendeleo ya wananchi wa jimbo lake. Kazi kubwa ya Mwakilishi wa CCM katika eneo hili ni kuhimiza bila kuchoka

utatuzi wa kero na shida za wananchi wa jimbo kwa moyo wa kujitegemea kulingana na uwezo uliopo Kijijini, Mtaani, Wadini, Katani, Wilayani na Mkoani.

(iv) Kuwafikishia wananchi wa Jimbo lake maagizo ya Serikali yanayotolewa mara kwa mara yakiwataka wayatekeleze; kuyafafanua vizuri maagizo hayo katika mikutano ya hadhara au mbele ya Serikali ya Mtaa, Kata/Wadi na Kijiji. Lengo hapa ni kuhakikisha kwamba kila agizo la Serikali limepokelewa na wananchi na limeeleweka ili waweze kulitekeleza kwa ukamilifu kama raia wema na waaminifu wa nchi yetu.

(v) Anawajibika kuhudhuria na kushiriki kwa ukamilifu katika vikao vyote vya Serikali na CCM vinavyomhusu.

(vi) Mbunge, Muwakilishi na Diwani wa CCM ajihusishe kwa ukamilifu na uimarishaji wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi inayohusika na uongozi wake na pia Chama kwa jumla.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya ngazi ya uongozi wa Mwakilishi anayehusika itafuatilia mara kwa mara utekelezaji wa wajibu wake huo, kuujadili katika vikao vyake na kutoa taarifa kwa vikao vya Chama vya ngazi za juu.

SIFA ZA WAGOMBEA

Ngazi ya Kitongoji hadi Wawakilishi/Bunge:

4. Kila raia wa Tanzania anayejitokeza kugombea nafasi ya uongozi Serikalini kwa tiketi ya CCM (ngazi ya Kitongoji hadi Wawakilishi/Bunge) sharti awe na sifa za jumla zifuatazo:-

(i) Awe mwanachama wa CCM asiyetiliwa shaka yoyote katika eneo lake, mwadilifu na anayekubalika na wananchi kwa jumla;

(ii) Awe na sifa zote zinazotakiwa na Katiba ya Nchi au Sheria au Kanuni inayohusu uongozi anaoutaka;

(iii) Awe anakubali kwa dhati imani, malengo, madhumuni na Sera za CCM;

(iv) Awe msitari wa mbele katika kuhudhuria vikao vya Chama vinavyomhusu kwa mujibu wa Katiba ya CCM;

(v) Awe mkweli, mwaminifu kwa CCM na mwenye tabia na mwenendo safi kwa jumla;

(vi) Awe mpenda maendeleo, mbunifu, hodari katika kazi na mwenye elimu, uzoefu na upeo mkubwa kuhusu maendeleo ya uchumi na jamii na ujenzi wa taifa kwa jumla.

Ngazi ya Rais

5. Sifa za mwanachama wa CCM atakayeteuliwa kugombea nafasi ya Rais wa Zanzibar, Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, zitawekwa rasmi na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM kwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

(i) Uzito wa nafasi hizo kwa nchi yetu.

(ii) Haja ya kulinda na kuendeleza mshikamano wa wana-CCM ndani ya Chama.

(iii) Haja na umuhimu wa kupanua demokrasia ndani ya CCM katika kuwapata viongozi wa Kitaifa; na

(iv) Hali halisi ya nyendo za ushindani wa kisiasa nchini.

Sifa za msingi zifuatazo zitazingatiwa:-

(1) Awe na uwezo mkubwa wa kuongoza Taifa kwa kuzingatia uzoefu wake katika uongozi wa shughuli za Serikali, Umma na Taasisi;

(2) Awe Mwadilifu, mwenye Hekima na Busara;

(3) Awe na angalau kiwango cha Elimu ya Chuo Kikuu au Elimu inayolingana na hiyo;

(4) Awe mwenye upeo na uwezo mkubwa wa kudumisha, kuimarisha na kuendeleza Muungano wetu, Umoja wetu, Amani na Utulivu wetu na Mshikamano wa Kitaifa;

(5) Awe mtu mwepesi wa kuona mbali, asiyeyumbishwa na mwenye uwezo wa kufanya uamuzi wa busara kuhusu masuala nyeti na muhimu ya taifa kwa wakati unaofaa;

(6) Awe na upeo mkubwa na usiotiliwa shaka kuhusu masuala ya Kimataifa ili aweze kuwa kiungo imara kati ya nchi yetu na Dunia yote kwa jumla;

(7) Asiwe mtu mwenye hulka ya udikteta au ufashisti bali awe mtu aneyeheshimu na kulinda Katiba ya Nchi, Sheria, Utawala Bora, Kanuni na Taratibu za Nchi;

(8) Awe mtetezi wa wanyonge, wa Haki za Binadamu, mzingatiaji makini wa maendeleo ya raia wote na asiwe na tamaa ya kujitafutia umaarufu wa mtu binafsi;

(9) Awe mstari wa mbele katika kuzifahamu, kuzieleza, kuzitetea na kuzitekeleza Sera za CCM na Ilani ya CCM ya Uchaguzi;

(10) Awe mpenda haki na awe mtu jasiri katika kupambana na dhuluma na maovu yote nchini;

(11) Asiwe ni mtu ambaye anatumia nafasi yake ya uongozi kujilimbikizia mali;

(12) Kwa jumla awe ni mtu anayekubalika na wananchi; na

(13) Awe mtu makini katika kuzingatia masuala ya uwajibikaji wa viongozi/watendaji na asiyevumilia uzembe katika utekelezaji wa majukumu/wajibu waliokabidhiwa ili kuinua nidhamu ya Kazi. Tija na Ufanisi.

6. Wagombea wa ngazi zote sharti wawe raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia ya mwaka 1995. Kwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano, sharti awe raia kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Na mgombea Urais wa Zanzibar, sharti awe raia kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Mzanzibari kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

FUNGU LA PILI

UTARATIBU WA KUOMBA UONGOZI

7. Ratiba ya Uchaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mdogo wowote unaofanyika, itawekwa na chombo cha Dola chenye mamlaka na madaraka ya kusimamia Uchaguzi nchini. Mara baada ya ratiba hiyo kutolewa, Katibu wa CCM wa ngazi inayohusika na uchaguzi huo atawapa fomu za kuomba uongozi wanachama wa CCM watakaojitokeza kugombea nafasi wazi iliyopo/zilizopo katika ngazi yake. Tarehe ya kuchukua na kurudisha fomu ataiweka kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya uchujaji na uteuzi wa wagombea ndani ya Chama.

8. Kila mwanachama wa CCM atakayechukua fomu atatakiwa kurudisha fomu yakekwa Katibu wa CCM anayehusika ndani ya muda uliowekwa, vinginevyo fomu yake haitapokelewa.

9. Utaratibu wa kuchukua na kurudisha fomu za wagombea uongozi kwa tiketi ya CCM utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Wanaogombea nafasi ya uongozi katika ngazi ya Kitongoji, Mtaa na Kijiji watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu wa CCM wa Tawi lenye nafasi hiyo ya uongozi.

(ii) Wanaogombea nafasi ya Diwani wa Kata (Bara) au Wadi (Zanzibar) watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu wa CCM wa Kata/Wadi inayohusika.

(iii) Wanaogombea nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Ubunge watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu wa CCM wa Wilaya inayohusika.

(iv) Wanaogombea nafasi ya Rais wa Zanzibar au Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watachukua fomu kutoka kwa Katibu Mkuu wa CCM na kuzirudisha kwa Katibu Mkuu wa CCM.

(v) Wanaogombea nafasi ya Diwani Viti Maalum Wanawake watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu wa Wilaya wa Jumuiya ya Wanawake inayoongozwa na CCM.

(vi) Wanaogombea nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi Viti Maalum Wanawake au Ubunge Viti Maalum Wanawake, watachukiua fomu na kuzirudisha kwa Katibu wa Mkoa wa Jumuiya ya wanawake inayoongozwa na CCM.

(vii) Fomu za kugombea zilipiwe kutoka ngazi ya Diwani hadi ngazi ya Rais. Kwa ngazi za chini, fomu zitolewe bure. Gharama ya kuchukua fomu iwe kama ifuatavyo:-

(a) Udiwani -Shs. 10,000/=.
(b) Ubunge/Uwakilishi-Shs.100,000/=
(c) Uspika wa BLW - Shs. 500,000/=
(d) Uspika wa Bunge - Shs. 500,000/=
(e) Urais -Shs.1,000,000/=

(viii) Mgao wa fedha uwe kama ifuatavyo ili kufanikisha maandalizi/kampeni za uchaguzi katika maeneo yanayohusika:-

Tanzania Zanzibar

(a) Udiwani - Wadi ipate 100%

(b) Ubunge/Uwakilishi - Jimbo lipate 50%
- Wilaya ipate 25%
- Mkoa upate 25%

(c) Uspika wa BLW - Afisi Kuu ipate 100%

(d) Urais wa Zanzibar - Afisi Kuu ipate 100%

Tanzania Bara

(a) Udiwani - *Kata* ipate 100%

(b) Ubunge - Jimbo la Uchaguzi ambalo ni Wilaya nzima lipate 75% na Mkoa upate 25%.
- Katika Wilaya yenye Majimbo mengi ya Uchaguzi, Jimbo lipate 50%, Wilaya ipate 25% na Mkoa upate 25%.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(a) *Uspika* wa Bunge - Makao Makuu ya Chama yapate 100%

(b) Urais wa Tanzania - Makao Makuu ya Chama yapate 100%.

UTARATIBU WA KURA ZA MAONI

10 (1) Mgombea yeyote wa CCM anayetaka kuingia katika chombo cha Dola, atateuliwa kwa kuzingatia kura za maoni zilizopigwa. Mgombea atakayeteuliwa ni yule aliyepata ushindi kwa wingi wa kura za maoni alizopata.

Isipokuwa kwamba endapo itathibitika kuwa kura hizo za ushindi alizipata kwa njia ya rushwa, kikao cha uteuzi wa mwisho hakitamteua kugombea nafasi anayoiomba.

(2) Endapo kwa sababu maalum, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itaona kwamba hakuna haja ya kuitisha kura za maoni kwa nafasi fulani, hususani katika uchaguzi mdogo, itakuwa na uwezo wa kuelekeza kwamba zoezi la kura za maoni lisifanyike.

(3) Utaratibu wa kupiga kura za maoni utakuwa kama ulivyoelezwa katika kanuni ya 18 ya Kanuni za Uchaguzi wa CCM.

11. Utaratibu wa kusimamia kura za maoni utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Katika ngazi ya Kitongoji, kura za maoni zitasimamiwa na viongozi wa watatu walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri kwa ajili hiyo na Kamati ya Siasa ya Tawi linalohusika. Wajumbe wote wa Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi watapangwa vizuri na Sekretarieti ya HalmashauriKuu ya Tawi ili kuratibu kazi hii katika Vitongoji vyote.

(ii) Katika ngazi ya Mtaa au Serikali ya Kijiji, kura za maoni zitasimamiwa na viongozi watatu walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri kwa ajili hiyo na Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi inayohusika.

Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Kata/Jimbo watapangwa vizuri na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Kata/Jimbo na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Wilaya ili waratibu kazi hii katika Mitaa yote na au Vijiji vyote.

(iii) Kwa nafasi ya Diwani wa Kata au Wadi, kura za maoni zitasimamiwa na Viongozi watatu wa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri na Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi. Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya watapangwa na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Wilaya katika Kata/Wadi ili waratibu kazi hii katika Matawi ya CCM ya Kata/Wadi inayohusika.

(iv) Kwa nafasi ya mjumbe wa Baraza la Wawakilishi/Mbunge, kura za maoni zitasimamiwa na viongozi watatu wa Halmashauri Kuu ya Wilaya walioteuliwa na kuandaliwa kwa ajili hiyo na Kamati ya Siasa ya Wilaya. Viongozi wawili wa Kamati ya Siasa ya Mkoa watapangwa na na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Mkoa kwenda katika kila Wilaya ya Mkoa unaohusika kuratibu shughuli zote za kura za maoni ili kuhakikisha kwamba upigaji kura unafanyika ipasavyo.

(v) Siku ya kupiga kura za maoni katika ngazi ya Kitongoji/Kijiji wana-CCM wa Mashina/Matawi ya kazini na Maskani/Mashina ya Wakereketwa, watapiga kura zao za maoni wakiwa katika Matawi ya Vijiji au Mitaa ambako wanaishi na ambako wao ni wanachama.

FUNGU LA TATU

UCHUJAJI NA UTEUZI WA WAGOMBEA

12. Utaratibu wa kuchuja na hatimaye kuteua mgombea/wagombea wa kila ngazi utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) **Ngazi ya Kitongoji:**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na mkutano wa Wanachama wote wa Shina/Mashina.

(2) Kamati ya Siasa ya Tawi ambamo Shina/Mashina yamo itawajadili wagombea.

(3) Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itafanya uteuzi wa mwisho wa mwana CCM atakayesimama kugombea nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Kitongoji kinachohusika.

(ii) **Ngazi ya Kijiji na Mtaa**

(1) Wagombea wote watapigiwa kura za maoni na Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi/Matawi.

(2) Kamati za siasa za Halmashauri Kuu za Matawi na Kata/Wadi zinazohusika zitawajadili wagombea.

(3) Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama watakaosimama kugombea Uenyekiti wa Mtaa, Ujumbe wa Kamati ya Mtaa, Uenyekiti wa Kijiji na Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

(iii) **Diwani wa Kata au Wadi:**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi inayohusika.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi linalohusika itawajadili wagombea.

(3) Kamati za Siasa za Kata/Wadi, Jimbo, Wilaya na Mkoa zitawajadili wagombea na kuwatolea mapendekezo yao.

(4) Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa mwanachama mmoja atakayesimama kugombea nafasi ya Diwani katika kila Kata au Wadi ambayo imo katika Mkoa unaohusika.

Katika kufanya kazi hiyo kwa upande wa Madiwani wanaomaliza muda wao, Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itazingatia pia tathmini iliyofanywa ya utendaji kazi wao katika kipindi kinachomalizika,.

(iv) **Ngazi ya Baraza la Wawakilishi/Bunge:**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na Mkutano Mkuu wa CCM wa kila Jimbo la Uchaguzi linalohusika,

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itawajadili wagombea.

(3) Kwa upande wa Tanzania Bara, Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itawajadili wagombea na kuwatolea mapendekezo yake kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Kamati ya Siasa ya Mkoa itawajadili wagombea na kuwatolea mapendekezo yake kwa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa ambayo nayo itatoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(4) Kamati Kuu itawajadili wagombea wote na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.
Katika kufanya kazi hiyo kwa upande wa Wabunge/Wawakilishi wanaomaliza muda wao, Kamati Kuu itazingatia pia tathmini itakayokuwa imefanyika ya utendaji kazi wao katika kipindi kinachomalizika.

(v) **Ngazi ya Diwani - Viti Maalum Wanawake**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na Mkutano Mkuu wa UWT Wilaya.
(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itawajadili wagombea na kuanda orodha ya majina kwa kuzingatia idadi inayotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi.
(3) Tume ya Uchaguzi itazingatia na kutangaza washindi ambao watakuwa sawa na asilimia 30 ya Madiwani wa Kata au Wadi ambao CCM imepata.

(vi) **Ngazi ya Uwakilishi/Ubunge - Viti Maalum Wanawake:**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na Mkutano Mkuu wa UWT Mkoa ambao utapendekeza majina matano ya kwanza kwa wingi wa kura ili yapelekwe mbele.

(2) Kamati za Siasa za Mikoa ya Tanzania Bara zitawajadili wagombea hao na kuwasilisha maoni/mapendekezo yao kwa Baraza Kuu la UWT Taifa. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, maoni na mapendekezo ya Kamati za Siasa za Mikoa yatawasilishwa kwa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa ili yakajadiliwe kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza Kuu la UWT Taifa.

(3) Baraza Kuu la UWT Taifa litawajadili wagombea na kuandaa orodha ya wagombea wote nchini kwa kuzingatia sifa za wagombea na umuhimu wa kuwa na mgombea/wagombea kutoka kila Mkoa.

(4) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itawajadili wagombea wote na kuwatolea mapendekezo yake.

(5) Halmashauri Kuu ya Taifa itateua wagombea kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi.

(6) Tume ya Uchaguzi itazingatia na kutangaza washindi ambao watakuwa sawa na asilimia 30 ya Wawakilishi/Wabunge wa Majimbo ambayo CCM imeshinda.

(vii) **Rais wa Zanzibar**

(1) Baada ya kujaza fomu, kila mgombea wa nafasi hii anatakiwa apate wadhamini 250 kutoka Mikoa isiyopungua mitatu ikiwemo angalau mkoa mmoja kutoa Pemba na mmoja kutoka Unguja.

Isipokuwa kwamba mjumbe yeyote wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mjumbe mwingine yeyote wa Mkutano Mkuu wa Taifa hataruhusiwa kumdhamini mgombea Urais wa Zanzibar.

(2) Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa itawachuja wagombea wote waliojitokeza na kutoa mapendekezo yake ya majina yasiyozidi matano kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa bila kuyapigia kura.

(3) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itapitia sifa za Wagombea hao na kutoa mapendekezo yake ya majina yasiyozidi **matatu** kwa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.

Isipokuwa kwamba endapo Kamati Kuu

itapendekeza jina moja tu, Halmashauri Kuu ya Taifa itapiga kura za "Ndiyo" au "Hapana"

(4) Halmashauri Kuu ya Taifa itapiga kura za siri kuchagua jina moja la mwanachama wa CCM atakayesimama katika uchaguzi wa Rais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM.

(5) Zoezi zima la uteuzi wa mgombea wa nafasi hii litafanyika na kukamilika angalau miezi sita kabla ya siku ya uchaguzi wenyewe iliyowekwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuhusu uchaguzi wa Rais wa Zanzibar.

(viii) **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:**

(1) Baada ya kujaza fomu, kila mgombea wa nafasi hii anatakiwa apate wadhamini 250 kutoka Mikoa isiyopungua 10, angalau miwili kati hiyo itoke Tanzania Zanzibar.

Isipokuwa kwamba mjumbe yeyote wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mjumbe mwingine yeyote wa Mkutano Mkuu wa Taifa hataruhusiwa kumdhamini mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itapitia sifa za wagombea wote na kutoa mapendekezo yake ya majina yasiyozidi matano kwa Halmashauri Kuu ya Taifa.

(3) Halmashauri Kuu ya Taifa itafikiria na kupiga kura za siri ili kupendekeza majina yasiyozidi matatu kwa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.
Isipokuwa kwamba endapo Halmashauri Kuu ya Taifa itapendekeza jina moja tu, Mkutano Mkuu wa Taifa utapiga kura za "Ndiyo" au "Hapana".

(4) Mkutano Mkuu wa Taifa utawapigia kura wagombea hao ili kuchagua jina moja la mwanachama wa CCM atakayesimama katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Mshindi atakuwa ni yule aliyepata zaidi ya asilimia 50 ya kura halali zilizopigwa.

(5) Zoezi zima la uteuzi wa mgombea wa nafasi hii litafanyika na kukamilika angalau miezi sita kabla ya siku ya Uchaguzi wenyewe iliyowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhusu uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(ix) **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

(1) Huyu atakuwa mgombea mwenza wa mwanachama wa CCM aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kusimama katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(2) Utaratibu wa kumpata Mgombea Mwenza utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano akitoka upande mmoja wa Jamhuri, Makamu wake atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.

(ii) Baada ya kumpata mgombea wa CCM wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, mgombea huyo atashauriana na Kamati Kuu juu ya mwana-CCM anayemfikiria awe mgombea mwenza (Makamu wa Rais).

(iii) Mgombea Urais atatamka jina la mgombea mwenza mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

(iv) Mgombea Urais akichaguliwa na wananchi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, mgombea mwenza atakuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Endapo nafasi ya Makamu wa Rais itakuwa wazi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atashauriana na Kamati Kuu juu ya mwana-CCM anayemfikiria awe Makamu wa Rais.

13. Wakati wa kura za maoni, ikitokea kwamba mgombea Udiwani/Uwakilishi/Ubunge ni mmoja, ateuliwe kugombea moja kwa moja kwa tiketi ya CCM bila ya kupigiwa kura za "Ndiyo" au "Hapana".

MALALAMIKO JUU YA UTEUZI WA WAGOMBEA

14. Mara baada ya matokeo ya uteuzi wa mwisho wa wagombea kutangazwa, mwanachama yeyote aliyeachwa kuteuliwa kugombea nafasi aliyoomba anaweza, endapo anayo malalamiko kuhusu uteuzi huo, kuwasilisha malalamiko yake kwa Katibu wa Chama wa ngazi yenye nafasi aliyoomba. Isipokuwa kwamba kama uteuzi unaolalamikiwa ni wa ngazi ya Taifa, malalamiko yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa CCM.

15. Malalamiko hayo yatawasilishwa kwa maandishi na lazima yaonyeshe kwa ukamilifu mambo yanayolalamikiwa. Jina na anwani ya mlalamikaji lazima vionyeshwe wazi katika barua ya malalamiko.

16. Malalamiko lazima yawasilishwe siku hiyo ya kutangazwa matokeo ya uteuzi ili kazi ya kuyasikiliza iweze kufanywa bila kuchelewa.

17. Wakati malalamiko yanasikilizwa, mgombea mteule anayelalamikiwa atakuwa anajiandaa ili asichelewe kuwasilisha fomu zake kwa Msimamizi wa Uchaguzi anayehusika.

18. Kwa kuwa shughuli za uchujaji na uteuzi wa wagombea wa CCM katika vyombo vya Dola ni sehemu ya kazi za Chama ndani ya Chama, malalamiko yote ya uteuzi yatamalizwa ndani ya vikao vya Chama haraka kadri inavyowezekana ili mgombea mteule asichelewe kuwasilisha fomu zake kwa Tume ya Uchaguzi siku ya kurudisha fomu (Nomination Day) na kusababisha CCM ikose mgombea kwa sababu ya malalamiko hayo. Katibu wa CCM wa ngazi inayohusika ahakikishe kwamba CCM haikosi mgombea kutokana na malalamiko.

19. Kwa ngazi za chini, kila Halmashauri Kuu ya CCM ya ngazi ya Katibu aliyepokea malalamiko, imepewa madaraka ya kuamua malalamiko yote juu ya uteuzi. Kwa ngazi ya Taifa, Kamati Kuu imepewa madaraka ya kuamua malalamiko yote ya uteuzi ambayo Katibu Mkuu wa CCM atapokea.

MIIKO YA SHUGHULI ZA UCHUJAJI NA UTEUZI WA WAGOMBEA

20. Maadili na Nidhamu ya Chama katika kusimamia na kutekeleza shughuli za uteuzi wa wagombea wa CCM katika vyombo vya Dola lazima vizingatiwe na wale wote wanaohusika. Hivyo yawapasa kuelewa na kuzingatia kuwa:-

(1) Ni mwiko kwa kiongozi yeyote kwa maneno au vitendo kumpendelea au kumsaidia kupata kura nyingi mwombaji mmoja dhidi ya mwingine miongoni mwa wale waliorudisha fomu.

(2) Ni mwiko kabisa kwa mgombea kutumia au kuhusisha ukabila, dini, rushwa, rangi, hila na eneo analoishi/analotoka katika shughuli yoyote ya uchaguzi.

(3) Ni mwiko kwa mgombea yeyote kufanya kampeni ya kupakana matope na ya aina nyingine yoyote ile dhidi ya mgombea mwingine.

(4) Ni mwiko kwa kiongozi yeyote au mwombaji yeyote wa nafasi ya uongozi au mwanachama yeyote aliyekabidhiwa dhamana ya usimamizi/uangalizi/uratibu wa kura za maoni, uchujaji na uteuzi, kufanya vitendo vya ukiukaji wa Kanuni hizi, Katiba ya CCM, Sheria, Ratiba na Taratibu za Uteuzi.

(5) Bila kuathiri haki ya mwanachama yeyote ya kutangaza wakati wowote nia yake ya kutaka kugombea nafasi fulani ya uongozi katika vyombo vya Dola, lakini kwa kuwa nafasi hizo zimewekewa muda maalum wa miaka mitano, kwa hiyo:-

(a) Ni marufuku kwa mgombea yeyote mtarajiwa au wakala wake, kufanya vitendo vyovyote vinavyoonekana dhahiri kuwa ni sehemu ya kampeni za kuwania nafasi anayoitafuta kabla ya muda rasmi wa uongozi unaohusika haujamalizika.

(b) Vitendo vya aina hiyo ni pamoja na utoaji wa misaada mbalimbali wakati uchaguzi unapokaribia, ambayo dhahiri ina lengo la kuvutia kura.

Isipokuwa kwamba Kanuni hii haitamhusu Rais, Mbunge, Mwakilishi, au Diwani ambaye yupo madarakani wakati huo, kwa kuwa yeye atakuwa bado anao wajibu wa kuhudumia eneo lake la uongozi.

(6) Ni marufuku kwa mgombea yeyote au wakala wake kuwaficha wajumbe wa mkutano wowote wa uchaguzi katika kambi maalum aliyoiandaa, ili wagombea wengine wasipate nafasi ya kuwaona wajumbe hao kuwaomba kura zao.

(7) Adhabu za kuvunja miiko iliyotajwa katika Kanuni hii ni hizi zifuatazo:-

(a) Kiongozi yeyote atakayethibitika kuvunja miiko hiyo atavuliwa uongozi wake.

(b) Mwanachama anayeomba kugombea nafasi yoyote atakayethibitika kuvunja miiko hiyo hatateuliwa kugombea nafasi anayoiwania.

FUNGU LA NNE

MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI WA VIKAO VYA UCHUJAJI NA UTEUZI WA WAGOMBEA

21. Ili haki iweze kutendeka wakati wa vikao vya kuchuja na au kuteua wagombea ni muhimu kuzingatia kwamba:-

(1) Wajumbe wa vikao vya uchujaji na uteuzi wa mwisho wa wagombea wasiwe na upendeleo wala ubinafsi katika kutoa uamuzi. Lengo Kuu la uteuzi liwe kumpata mwana - CCM mwenye uwezo mkubwa wa uongozi na anayekubalika na wananchi ili ateuliwe kugombea nafasi ya uongozi iliyopo.
Hivyo kura za maoni lazima zizingatiwe kwa kadri inavyopasa. Isipokuwa kwamba kama kuna lalamiko lolote au utata kuhusu nani ateuliwe kugombea nafasi wazi iliyopo (ukiondoa nafasi ya Rais), Kamati Kuu kwa niaba ya Halmashauri Kuu ya Taifa itakuwa na uamuzi wa mwisho juu ya suala hilo kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Wajumbe hawana budi kuepuka kutoa siri za vikao baada ya kukamilisha kazi ya kuwajadili wagombea. Matokeo ya uteuzi wa mwisho yatolewe au yatangazwe na mhusika kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa. Mjumbe atakayevunja kifungu hiki cha Kanuni atadhibitiwa na Chama Cha Mapinduzi.

(3) Wajumbe wa vikao vya uchujaji na uteuzi wa wagombea kwa ngazi inayohusika hawaruhusiwi kuendelea na kazi ya uchujaji na uteuzi iwapo wao ni wagombea katika ngazi hiyo. Akidi ya wajumbe ikipungua, na kwa kuwa hili litakuwa limefahamika mapema kabla ya kikao, Halmashauri Kuu ya ngazi hiyo iteuwe wajumbe wengine kutoka miongoni mwao wa kukamilisha akidi. Idadi ya watakaoteuliwa ilingane na ya wajumbe waliozuiwa kushiriki kwa kuwa ni wagombea.

(4) Wajumbe wa vikao vya uteuzi wazingatie kwa makini nidhamu na maadili ya vikao vya CCM.

"**Inawezekana, timiza wajibu wako."**
(Baba wa Taifa, Mwl. J.K. Nyerere)